



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.HA.92/243/01/66

Tarehe: 29 Agosti, 2025

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya uwekezaji na Ukanda maalum wa kiuchumi (TISEZA),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

Yah: **OMBI LA KUTOKUWA NA PINGAMIZI LA UTOAJI WA CHETI CHA UWEKEZAJI
KATIKA KIWANJA NA. 336 KITALU "A" KEREGE WILAYA YA BAGAMOYO**

Tafadhali husika na kichwa habari hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo imepokea barua yenye **Kumb.Na.PML/06/MHB/2025** ya tarehe **07 Agosti, 2025** kutoka Kampuni ya **Pioneer Metals Limited** ya kuomba kupata barua ya kutokuwa na pingamizi kwa mradi utakaofanyika katika kiwanja tajwa ili Ofisi yako iweze kutoa Cheti cha Uwekezaji.
3. Vilevile, barua yao imeeleza kuwa, walipo fuatilia ili kupata Cheti cha Uwekezaji katika Ofisi yako walielekezwa kupata kwanza barua ya kutokuwa na pingamizi la uwekezaji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Pia wamewasilisha nakala ya mkataba wa manunuzi ambao unaonyesha wamenunua eneo hilo kutoka kwa Ndugu Obedi Solomon Kimaro.
4. Aidha, kulingana na Mchoro wa Mipangomiji wa eneo husika, mchoro **Namba 19/BGY/1413/082019, 19/BGY/1414/082019 & 19/BGY/88/062010B** matumizi ya kiwanja ni kwa ajili ya Biashara,

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S. L. P. 59, 61301 BAGAMOYO, Mkoa wa Pwani.

Simu Na: +255733860575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz, barua@bagamoyodc.go.tz

Tovuti: www.bagamoyodc.go.tz

5. Hivyo, Ofisi haina pingamizi kwa uwekezaji utaofanyika katika kiwanja tajwa kwa kuzingatia matumizi yaliyoainishwa katika mchoro wa Mipangomiji wa eneo husika pia, Kampuni hiyo itapaswa kukamilisha taratibu za kupata umiliki kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania kwakuwa Kampuni hiyo ni ya kigeni.

6. Ahsante.



Shauri Selenza
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO
S.L.P. 59
BAGAMOYO

Nakala:- Mkurugenzi,
Irvines Tanzania Limited,
S.L.P 39997,
DAR ES SALAAM.

– Kwa taarifa

Mkurugenzi,
Future Century Limited,
S.L.P 301,
BAGAMOYO.

– Kwa taarifa